

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA



BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

ORODHA YA MAJINA YA WANACHAMA HAI WA PSPTB KITAALUMA
(PSPTB ACTIVE MEMBERS)

Dodoma Oktoba 19, 2026.

Bodi ya wataalam wa ununuzi na ugavi (PSPTB) ni taasisi ya serikali iliyopo chini ya wizara ya Fedha, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya PSPTB Sura ya 179 ya Sheria za Tanzania. PSPTB ni chombo cha kisheria chenye mamlaka ya kusimamia na kudhibiti viwango vya kitaaluma, mwenendo na maadili ya kitaaluma katika taaluma ya mnyororo wa ugavi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(g) cha Sheria ya PSPTB, Bodi hii imepewa mamlaka ya kipekee ya kusajili watu waliokidhi vigezo vya kitaaluma na kuwapa mamlaka ya kisheria ya kufanya kazi za kitaalamu katika Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

Pia, kwa mujibu wa kanuni ya 38(1)(b) ya Kanuni za PSPTB 2009, Bodi inaweza kumfuta mtu ambae ameshindwa kulipa ada zaidi ya miezi 24. Hadi kufikia tarehe 15 Oktoba 2026, jumla ya wanachama hai wa PSPTB kitaaluma waliokidhi vigezo vya kufanyakazi za Ununuzi na Ugavi ni 4,449 kati ya jumla ya wataalam **22,269** wa ununuzi na ugavi waliosajiliwa.

Kutokana na kanuni tajwa hapo juu, PSPTB inautaarifu umma kuwa itaweka orodha ya majina ya wanachama hai wa PSPTB Kitaaluma (*PSPTB Active Members*) kwenye tovuti yake ambao kisheria ndio watakaostahili kufanya kazi za ununuzi na Ugavi na sio vinginevyo.

Hata hivyo, PSPTB itaendelea kutoa orodha ya majina ya wanachama hai wa PSPTB kitaaluma (*PSPTB active members*) kwenye tovuti yake kila wiki kuongeza majina ya wataalam watakao kuwa wamekidhi vigezo.

PSPTB inatoa rai kwa waajiri wote wa sekta za umma na binafsi kuhakikisha kuwa kazi za ununuzi na ugavi zinafanywa na wataalam ambao majina yao yamewekwe kwenye tovuti ya PSPTB na sio vinginevyo.

Kwa yeyote atakayepata changamoto tafadhali awasiliane na PSPTB kwa simu namba **0738 441 971** au **0737 157312**.

Imetolewa na :